


20 Machi 2020



Tume ya Ushindani Yachukua Hatua Kulinda Walaji Katika Kipindi Hiki cha Mlipuko wa Corona

- Tume ya Ushindani Tanzania imewaonya waagizaji, wafanyabiashara, wazalishaji, wasambazaji wa dawa za kutakasa mikono na maeneo yanayoweza kuguswa kwa mikono, barakoa na vizuizi vya mikono/glovu.
- Uchunguzi wa awali unaonyesha bei ya bidhaa hizo kupanda maradufu baada ya mlipuko wa corona
- Kupanga bei baina ya washindani, kuficha, kupunguza, au kukataa kusambaza sokoni bidhaa kwa lengo la kupandisha bei na kujipatia faida kubwa isivyo halali, na vitendo hadaifu dhidi ya walaji wa bidhaa kuhusiana na uhalisia na usahihi wa aina ya bidhaa.

Tume ya Ushindani Tanzania inakuwa moja kati ya mamlaka chache Barani Afrika kuonya waagizaji, wafanyabiashara, wazalishaji, wasambazaji wa dawa za kutakasa mikono na maeneo yanayoweza kuguswa kwa mikono, barakoa na glovu kuwa kujipangia bei, kuficha, kusababisha uhaba, kukataa kuuza bidhaa husika wakati wa janga la corona ni kosa chini ya Sheria ya Ushindani ya 2003.

Mnamo tarehe 19 Machi 2020, Mkurugenzi Mkuu wa Tume ya Ushindani, Dk. John Mduma alionya kwamba kumekuwa na malalamiko juu ya uhaba na upandishwaji bei kinyemela wa bidhaa husika. Onyo linasomeka, "Tume ya Ushindani imechunguza na kubaini kuwa malalamiko hayo ni ya kweli, inawakumbusha waagizaji, wafanyabiashara, wazalishaji na wasambazaji kwamba Tume ya Ushindani inakataza udanganyifu katika biashara kama vile kupandisha bei kiholela, na mengineyo,"

Kifungu cha 9 cha Sheria ya Ushindani inabainisha kwamba:

9.- (1) Ni marufuku mtu yoyote kufanya au kutekeleza makubaliano ambayo lengo lake au matokeo yake ni: (a) kupanga bei kati ya washindani; (b) washindani kula njama ya kukataa kusambaza bidhaa; au (c) kula njama katika kuomba zabuni au ugavi. (2) Katika kifungu hiki:

(a) "kula njama ya kukataa kusambaza bidhaa baina ya washindani" kuna maanisha kupanga, kuzuia au kudhibiti bei, ushuru au tozo zingine kwa, au vigezo au masharti ambayo, muhusika katika makubaliano atasambaza au kupata, au kuomba kusambaza au kupata, bidhaa au huduma, katika ushindani na muhusika mwingine yeyote katika makubaliano;

(b) "washindani kula njama ya kukataa kusambaza bidhaa" inamaanisha:

(i) kuzuia muhusika katika makubaliano kusambaza bidhaa au huduma kwa watu fulani, au kununua bidhaa au huduma kutoka kwa watu fulani, katika ushindani na muhusika mwingine yeyote kwenye makubaliano;

(c) "vizuizi vya pato kati ya washindani" maana yake ni kuzuia, kukwaza au kudhibiti uzalishaji wa muhusika mmoja katika makubaliano ya bidhaa au huduma zinazotolewa, katika ushindani na muhusika mwingine yeyote kwenye makubaliano;

For further information on legal updates please contact:

E: info@fbattorneys.co.tz

About FB Attorneys

FB Attorneys is an all service law firm based out of Dar es Salaam, Tanzania.

We cover all aspects of the law and specialise in all corporate and commercial matters including Mining, Oil & Gas, Tax, Litigation, Competition, Banking & Intellectual Property law.

FB Attorneys has been ranked as a tier 1 law firm by the IFLR 1000 in the Energy & Infrastructure and Financial & Corporate sectors, tier 1 by Legal 500 and band 1 by Chambers and Partners General Business Law.

FB Attorneys

8th Floor, Amani Place, Ohio Street
P. O. Box 19813
Dar es Salaam, Tanzania
T: +255 22 2135994/5
E: info@fbattorneys.co.tz
W: www.fbattorneys.co.tz

Disclaimer

Information found in this legal update and any attachments are confidential and may be privileged or otherwise protected from disclosure, and intended solely for the use of the individual or entity to whom it is addressed to. If you are not the intended recipient, please notify the sender immediately and delete this message and any attachment from your system. Any views or opinions expressed in the message or its attachments are not necessarily those of FB ATTORNEYS.

© FB Attorneys 2020. All rights reserved.



FB Attorneys



2019



2019

PROUD MEMBER OF



Lawyers for Africa • Advogados para Africa
• Avocats/Conseils pour l'Afrique

LEGAL UPDATE

FB ATTORNEYS

20 Machi 2020

Chini ya Sheria ya Ushindani, makosa yaliyotajwa hapo juu yanaweza kusababisha kutolewa kwa maagizo ya kufuata utaratibu na au adhabu kali hutolewa, hadi asilimia 10 ya mapato ya mkosaji. Adhabu kama hizo zinaweza kutolewa kwa kipindi cha miaka 6 kutoka tarehe ya kosa husika na uzoefu unaonyesha kuwa Tume ya Ushindani haiogopi kuchukua hatua kali.

Hatua hii ya Tume ya Ushindani ni muhimu katika kipindi hiki ambacho walaji wanapambana na athari za virusi vya corona.

Katika taarifa yake, Tume ya Ushindani imetoa namba ya simu kwa ajili ya kupiga na kutoa taarifa ili kupambana na tabia inayozuia ushindani wa kibiashara. Watumiaji wanaweza kupiga simu ya bure kwa namba ifuatayo:

Simu: 0800110094 au barua pepe: info@competition.or.tz

Kusoma toleo la Kiswahili la Ilani ya Tume ya Ushindani [bonyeza hapa](#).

For further information on legal updates please contact:

E: info@fbattorneys.co.tz

About FB Attorneys

FB Attorneys is an all service law firm based out of Dar es Salaam, Tanzania.

We cover all aspects of the law and specialise in all corporate and commercial matters including Mining, Oil & Gas, Tax, Litigation, Competition, Banking & Intellectual Property law.

FB Attorneys has been ranked as a tier 1 law firm by the IFLR 1000 in the Energy & Infrastructure and Financial & Corporate sectors, tier 1 by Legal 500 and band 1 by Chambers and Partners General Business Law.

FB Attorneys

8th Floor, Amani Place, Ohio Street
P. O. Box 19813
Dar es Salaam, Tanzania
T: +255 22 2135994/5
E: info@fbattorneys.co.tz
W: www.fbattorneys.co.tz

Disclaimer

Information found in this legal update and any attachments are confidential and may be privileged or otherwise protected from disclosure, and intended solely for the use of the individual or entity to whom it is addressed to. If you are not the intended recipient, please notify the sender immediately and delete this message and any attachment from your system. Any views or opinions expressed in the message or its attachments are not necessarily those of FB ATTORNEYS.

© FB Attorneys 2020. All rights reserved.



FB Attorneys



2019



2019

PROUD MEMBER OF

